## HABARI ZA KUTOKA KWA WAANDISHI WA ISAAA

**Maoni yaliyotolewa na Dkt Clive James, Mwenyekiti wa ISAAA, Juni 2012 kuhusu Taarifa ya USDA ya Mazao kwa Ekari.**

**Taarifa ya USDA kuhusu Mazao kwa Ekari ya 2012, imethibitisha kuwa wakulima wa Marekani wameendelea kuonyesha imani kubwa kabisa na mategemeo katika mazao ya kibayoteki.**

*Ukubalifu wa mazao ya kibayoteki kiutandawazi unategemewa kuendelea kukua siku zijazo, hasa katika nchi zinazoendelea, kuna matarajio ya maandalizi ya bidhaa mpya.*

Manila, Agosti 17, 2012 – Dkt James alisema kwamba wakulima wa Marekani wameendelea kuonyesha mategemeo ya kipekee ya mazao ya kibayoteki / ugeuzaji jeni, yaliyobadilishwa kwa kupitia bayotekinolojia. Taarifa ya Juni 2012 kuhusu mazao kwa ekari ya USDA inaonyesha kuwa teknolojia hii ya kisasa imekaribia uzuri au kuwa bora kabisa katika mazao matatu ya kibayoteki ya maeneo makubwa – mahindi, maharage ya soya na pamba – mazao yaliyofanywa ya kibiashara huko Marekani mwaka 1996.

“Viwango vikubwa vya pekee vya ukubalifu ni ushahidi wa imani kubwa kabisa na mategemeo ya mazao ya kibayoteki na mamilioni ya wakulima ulimwenguni mwote” akasema Dkt Clive James, Mwanzilishi na Mwenyekiti wa Shirika la Kimataifa la Upataji na Utumizi wa Kilimo cha Kibayoteki (ISAAA) . “Wakulima ni mabingwa wa kudhibiti hatari za kuudhi. Mara tu mazao ya kibayoteki yatakapofanywa ya kibiashara, ukubalifu wake utakuwa wa haraka na utafanywa mzuri au kuwa bora kabisa – sababu iliyo rahisi ya ushindi wa mazao ya kibayoteki huko Marekani, na katika nchi zingine 28 za ulimwengu, ni kuwa hutoa faida muhimu na za aina nyingi kwa kupunguza hasara za mavuno zinazotokana na vijidudu, magugu na magonjwa, na pia husababisha uokoaji mkubwa wa dawa za kunyunyuzia.”

Katika Taarifa ya USDA ya Juni kuhusu Mazao kwa Ekari, Dkt James alizingatia kuwa, taarifa inaonyesha kukaribia uzuri au ubora kabisa wa teknolojia hii katika mazao makuu matatu ya Marekani, ya 88% ya mahindi yote, 93% ya maharage ya soya yote, na 94% ya pamba ya nyanda za juu yenye aina mbalimbali za kibayoteki zinazolimwa na mahuluti zikionyesha sifa kuu bainishi za kuzuia wadudu na kuhimili sumu ya mimea.

Tangu mazao ya kibayoteki yalipoanza kufanywa ya kibiashara mara ya kwanza huko Marekani, na nchi tano zingine mwaka 1996, mamilioni ya wakulima kwenye nchi 29 ulimwenguni mwote zilifanya maamuzi ya kupanda na kuyapanda tena mazao yanayoonyesha teknolojia kwenye mkusanyiko wa eneo la zaidi ya hekta bilioni 1.25 au ekari bilioni tatu – eneo kubwa zaidi la ardhi iliyopandwa kwa asilimia 25 kubwa zaidi ya fungu lote la Marekani. Data za ISAAA zinaonyesha kuwa wakulima wa Marekani wanaendelea kupanda mazao zaidi ya kibayoteki kuliko nchi yoyote ingine ulimwenguni mwaka 2011- jumla ya karibu hekta milioni 70 au ekari milioni 170, ambazo kati ya hizo nusu yake ni eneo la mahindi; na mbili kwa tatu ya pamba ilikuwa na sifa bainishi zaidi ya moja, inayozalisha faida nyingi.

Kwa kuongezea mazao makuu matatu ya kibayoteki mahindi, maharage ya soya na pamba Marekani pia ilikuza nusu milioni ya hekta za kiazi sukari (ukubalifu wa asilimia 95% uliopatikana katika miaka 5 – kiwango cha haraka zaidi cha ukubalifu katika Marekani) na maeneo ya wastani ya kihekta ya kanola, majani ya alfa alfa, boga na papaya. Ukame mharibifu wa sasa huko Marekani, ambao unaathiri japo nusu ya zao la mahindi, umekuza ongezeko la ari katika mahindi ya kibayoteki yanayohimili ukame ambayo kwa sasa yanajaribiwa kwenye mashamba makubwa ya majaribio. Ni mapema mno kuanza kujadili ubora wa mahindi ya kibayoteki yanayohimili ukame hadi tathmini za data kutoka kwenye mashamba ya majaribio huko Marekani zitakapokamilika baadaye mwaka huu. Sifa bainishi inayohimili ukame ni ngumu zaidi kufahamika (changamani) kuliko mimea inayohimili sumu na inayozuia wadudu na maendeleo yake huenda yakawa ya msingi wa hatua kwa hatua. Matokeo ya kutia moyo kutoka mashamba ya majaribio ya 2012 huko Marekani ya

mahindi ya kibayoteki yanayohimili ukame itakuwa ni hatua ya mbele na ya maana katika kushughulikia ukame, kikwazo kikubwa zaidi dhidi ya kuongezea uzalishaji wa zao kiutandawazi, ambapo mazao yote ya kijadi na yale ya utumizi wa kibayoteki yanaweza kuchangia.

Dkt James alisema kuwa "mwelekeo wa kwenda juu unategemewa kufikia viwango vya mategemeo mazuri ya ukubalifu wa kiasi cha asilimia 90 ambacho tumekiona huko Marekani, pia kimekuwa ni dhahiri kwenye nchi zingine za viwanda kama Australia kwa asilimia 95.5% ya ukubalifu kwenye pamba ya kibayoteki. Hivyo hivyo, kama ilivyotegemewa, mazao makubwa ya kibayoteki katika nchi kuu zinazoendelea zinaonyesha mwelekeo sawa na huo kwa mara nyingine zinathibitisha imani na mategemeo ya wakulima kwenye teknolojia hii.

Maharage ya soya yanayohimili sumu ya mimea imefikia asilimia 100% huko Ajentina na data za hivi karibuni zaidi za 2011 zinaonyesha pamba huko India imefikia hadi asilimia 88%, na maharage ya kibayoteki huko Brazili asilimia 83%. Ukichukulia kuwa bidhaa katika masoko ya zamani tayari yana mwelekeo wa kuenda juu karibu kufikia viwango vizuri zaidi, ongezeko la kila mwaka la ukuaji wa ukubalifu utakuwa wa kadiri na utaweza kuongezewa nguvu kwa;

1) Kupanda maeneo zaidi ya hekta; kama ilivyokuwa kwenye upandaji wa jumla wa mahindi huko Marekani mwaka 2012 (zaidi kwa 5%);
2) Sifa bainishi mpya au mazao mapya ya kibayoteki kuidhinishwa; au
3) Nchi mpya zinakubali mazao ya kibayoteki".

**Kiwango na kipimo cha ukubalifu katika nchi zinazoendelea inazima ile ya mataifa ya viwanda.**

Dkt James alitambua kuwa kati ya nchi 29 ambazo zilikubali mazao ya kibayoteki mwaka 2011, nchi 19 zilikuwa nchi zinazoendelea na nchi 10 zilikuwa za mataifa ya viwanda. Uchina na India zinaongoza katika ukubalifu wa Asia. Brazili na Ajentina zinaongoza katika ukubalifu wa Amerika Kusini na Afrika Kusini inaongoza katika

ukubalifu wa bara la Afrika.  Kiwango cha ukuaji wa mazao ya kibayoteki katika nchi zinazoendelea cha asilimia 11, au hekta milioni 8.2 mnano 2011, ulikuwa wa kasi mara mbili na mkubwa mara mbili sawa na nchi za viwanda kwa asilimia 5 au hekta milioni 3.8.

Nchi zinazoendelea zilipanda takribani asilimia 50 ya mazao ya kibayoteki mwaka 2011 kiutandawazi na zinatarajiwa zishinde eneo la ardhi ya nchi za viwanda zilizotengwa kwa mazao mwaka 2012, Dkt. James alisema.  Kwa kuongezea, zaidi ya asilimia 90 ya wakulima wanaopanda mazao ya kibayoteki ulimwenguni mwote (sawasawa na zaidi ya wakulima milioni 15) ni wakulima maskini wasio na mtaji katika nchi zinazoendelea, zaidi kwa asilimia 8 au milioni 1.3 kuanzia 2010, aliongezea.

Dkt James alisema kuwa katika kipindi cha karibuni,  nchi kinara kubwa zaidi kwa mazao ya kibayoteki kiutandawazi itakuwa Brazili ikifuatiwa na Uchina mara uidhinishaji wa mahindi ya kibayoteki ya kibiashara utakapofanywa, ambao unaweza kuwa mapema 2013.  Brazili, nchi ya pili baada tu ya Marekani kwa jumla ya eneo la ardhi iliyopandwa mazao ya kibayoteki, ina msingi wa kisayansi; ulio bora na wenye mtindo wa haraka wa kufuatilia ukubalifu wa mazao ya kibayoteki pia itafaidika kutokana na njia mpya ya mazao ya kibayoteki kutoka mataifa yenye kubadili, ubia wa umma na wa kibinafsi na asasi ya sekta yake ya uchunguzi ya EMBRAPA, Dkt james aliongezea.  Brazili tayari imeidhinisha, kwa mara ya kwanza, maharage ya kibayoteki yenye “sifa za pamoja” za kuhimili sumu ya mimea na zinazozuia vijidudu na hatua za kuifanya ya kibiashara ingeweza kuanza mapema kama mwishoni mwa 2012 wakati ambao upandaji hufanywa huko kusini mwa Ikweta.  Uchina tayari ina wakulima wadogo milioni 7 wanaokuza pamba ya kibayoteki kwa ufanisi na hivi karibuni imetoa kipao mbele kwa mahindi ili Uchina iweze kufaidika kutokana na uimarishaji mahindi yake ya kibayoteki yatakayoongeza bidhaa za nyama na kuifanya nchi hiyo ijitegemee na ijitosheleze zaidi katika malisho ya wanyama.  Jinsi uchina inavyokuwa maarufu, nyama zaidi zinaliwa ambazo nazo huleta mahitaji zaidi ya mazao ya malisho, mahindi na maharage ya soya. Baada ya mwongo mmoja wa

maendeleo, uidhinishaji wa “Mchele wa Kikahawia”, unategemewa huko Ufilipino mwaka 2013/14. Bidhaa hii muhimu inao uwezo wa kuzalisha manufaa ya kuokoa maisha ya binadamu – kiasi cha watu 6,000 kwa siku, wengi wakiwa wanawake na watoto, ambao hufa kwa kutokana na matatizo yanayosababishwa na upungufu wa vitamini A.

Kwa kuhitimisha, Dkt James alizingatia kuwa katika bara la Afrika, Afrika kusini imepanda mahindi ya kibayoteki kwa ufanisi, maharage ya soya, na pamba kwa zaidi ya mwongo mmoja, na Burkina Faso inalima pamba Bt, na Misri, mahindi Bt. Nchi kadhaa za kiafrika, zikiwemo Uganda, Kenya, na Nigeria zina mashamba ya majaribio kwa lengo la matayarisho ya mazao ya kibayoteki na kuwa zao la pamba lililokubaliwa kwa mapana huenda likawa la kwanza kufanywa la kibiashara.
Mashamba ya majaribio ya kibayoteki huko Afrika ni pamoja na pamba, mahindi, ndizi, mbaazi, mihogo na viazi vitamu.

Shirika la Huduma la Upataji na Utumizi wa Kilimo cha Kibayoteki (ISAAA) ni shirika lisilo la faida lenye mtandao wa vituo vya kimataifa lililoundwa kuchangia katika kupunguza njaa na umaskini kwa kushirikiana katika ujuzi na utumizi wa kilimo cha bayotekinolojia. Clive James, mwenyekiti na mwanzilishi wa ISAAA, aidha amekuwa na/au akiishi kufanya kazi kwa miaka 30 iliyopita kwenye nchi zinazoendelea za Asia, Amerika kusini na Afrika, akitoa nguvu zake kwenye utafiti wa kilimo na masuala ya kimaendeleo akiangazia kilimo cha bayotekinolojia na usalama wa chakula kiutandawazi. Kwa maelezo zaidi kuhusu ISAAA na utafiti wake angalia knowledge.center@isaaa.org